# JUKWAA LA UCHUMI

## Undani wa mama aliyefanikiwa kiuchumi kwa kuokota makopo

NA WARIOBA IGOMBE

MWANAZAINA Hamisi maarufu kwa Zainabu ni mwanamke aliyeonyesha uthubutu, baada ya kuamua kutokuwa tegemezi kwa kuiona fursa ya kuokota makopo ya chupa za plastiki kama njia sahihi kujikwamua kiuchumi.

Mwanazaina umri wa miaka 38 ni mama wa watoto watatu mkazi wa Mtaa wa Oilcom Kata ya Tungi, Manispaa ya Morogoro, akizungumza na mwandishi wa makala hii, alisema alikuwa anajihusisha na kazi ya mama lishe, maeneo ya Masika na Msamvu, ambayo haikumpa faida.

Alisema akiwa mama lishe, alikutana na baadhi ya wanaume waliokuwa wakuokota makopo, baada ya kuchunguza aligundua kazi hiyo ina faida, kubwa pia inaweza kufanywa na mwanamke.

"Mwaka 2019 nilIacha kazi ya mama lishe na kuanza kuokota mapoko ya chupa za plastiki, nilikuwa nikizikusanya na kuzipekeka kwa wakala wa chupa hizo kazi niliyoifanya kwa moyo wangu wote,"alisema.



Watu wanaomfahamu walipokuwa wakimuona anaokota makopo mitaani, wakati alikuwa mama lishe, walihisi amechanganyikiwa akili lakini haikubwa kweli, baadaye watu hao watamuelewa dhumuni lake la kuokota makopo.

Mama huyo alisema akiwa anaendelea na kukusanya chupa za maji, zilizokwisha tumika aliamua kuwekeza nguzu zake zote katika kazi hiyo kwani aliamini kuwa ipo siku atapata mafanikio makubwa.

Alisema kilichomsukuma kufanya kazi hiyo ni baada ya kuona, kuna chupa nyingi za plastiki mitaani, hali ambayo ilikuwa ikisababisha uchafunzi wa mazingira.

"Baada ya kuona nina mtaji wa sh. 100,000 niliamua kuachana na kazi ya kuokota makopo (chupa za plastiki) na kuanza kununua bidhaa hiyo kutoka kwa watu wengine, kazi ambayo imenipa mafanikio makubwa na sasa najivunia,"alisema Mwanazaina.

Mwanasaina alisema mafaniko ya kazi yake hiyo ni pamoja na kupata mume aliyempata wakati akiokota makopo na hiyo ni baada ya mume huyo kumuona mama huyo ni mchakalikaji, anayejua thamani ya fedha na anaitafuta kwa jacho lake.

"Nikiwa naokota chupa za plastiki nilikutana na kijana ambaye, alinipenda baada ya kuona nimeamua kufanya kazi hiyo, kwa wakati huo sikuweza kumkubalia hadi pale nilipojiridhisha kuwa siyo tapeli ndipo nilipomkubalia na hivyo tukamua kufunga ndoa,"anasema Mwanazaina.

> **"Nikiwa naokota chupa za plastiki nilikutana na kijana ambaye, alinipenda baada ya kuona nimeamua kufanya kazi hiyo, kwa wakati huo sikuweza kumkubalia hadi pale nilipojiridhisha kuwa siyo tapeli ndipo nilipomkubalia na hivyo tukamua kufunga ndoa...**
>
> **Mwanazaina Hamisi, mjasiriali wa makopo ya plastiki.**

Mbali na mafaniko hayo ya kupata mume, pia kazi hiyo imeniwezesha kupata kiwanja, kusomesha watoto akiwemo mmoja wa kike anayesoma kidato cha tano huko mkoani Tanga,

Alisema alianza na mtaji wa sh. 100,000, lakini sasa ana zaidi ya sh. milioni tatu lengo lake ni kumiliki kiwanda cha kuchakata chupa hizo za plastiki, kufungua fursa kwa vijana, hususan wa kike kupata ajira na kuwa na uhakika wa kupata kipato..

Alisema mafaniko mengine ni kuweka mazingira katika hali ya usafi, kwani kitendo cha kununua bidhaa za plastiki ni moja ya njia ya kusafisha mazingira, ambayo yanatuzunguka maeneo mbalimbali ya mitaa ndani na nje Manispaa ya Morogoro.

Chupa hizo zisingekuwa na soko mazingira yetu yasingekuwa salama, ingechangia kuhatarisha usalama wa viumbe hai. Mbali na chupa hizo kuwa na soko, lakini bado uchafuzi wa mazingira utokanao na chupa hizo upo, kwani baadhi ya watu wamekuwa wakitumia vinywaji vya chupa hizo kisha kutupa ovyo.

"Soko la chupa hizo lipo hasa kwa chupa nyeupe, chupa za rangi ya kijani na nyeusi hizo hazina soko kabisa na hivyo haziokotwi na waokota makopo, tunaiomba serikali iingilie kati suala hili viwanda vya kuchakata bidhaa za plastiki vianze kununua, kwani bila hivyo uchafunzi wa mazingira wa chupa za rangi ya kijani na nyeusi utaendelea na kuleta athari kwa jamii,"alisema.

Mwanazaina alisema hakuna mafinikio yasiyokuwa na changamoto, katika kazi yake hiyo inatokana na viwanda vya kuchakata hususan vya Mkoa wa Morogoro, kununua bidhaa hiyo kwa bei ya reja reja na siyo ya jumla.

Alisema kitendo cha viwanda vya kuchakata plastiki vipo viwili Manispaa ya Morogoro, hununua bidhaa hiyo kwa bei ya rejareja badala ya jumla, ni hasara kutokana na wao kutokuwa na sehemu ya kusemea kero yao, wamekuwa wakiuza kwa njia hiyo.

Alisema chupa za plastiki zimekuwa zikitapakaa kila kona ya nchi ,hususan katika miji mikubwa hivyo kutokana uwepo wao serikali ,ingewatazama mawakala wote wanaonunua chupa hizo, kwa jicho la tatu kwani wanasaidia kutunza mazingira kwa ujumla.

Mwanazaina alisema ana matarajio ya kumiliki kiwanda cha kuchakata bidhaa zote za plastiki, kutoa fursa kwa vijana kupata ajira, ametaka wanawake kuacha tabia ya kukata tamaa ya kimaisha au kubweteka na badala yake wafanye kazi halali kwa na kujituma kwani kutawafanya wapate maendeleo.

"Baadhi ya kina mama hapa Morogoro wamekuwa wakijihusisha na biashara haramu, ikiwemo ya ngono,i wanaona kufanya kazi ngumu kama mimi hapa ni mateso kwao, ni fikra potofu na kamwe hawawezi kufanikiwa hivyo wanatakiwa kujitoa kikamilifu kupambana kimaisha,"alisema.

Alen Charles ni mume wa Mwanazaina, anampongeza mkewe kwa kuonyesha uthubutu kufanya kazi hiyo, ambayo imezoeleka kufanywa na wanaume, alisema ataendelea kumuunga mkono kufikia ndoto yake ya kumiliki kiwanda cha kuchakata bidhaa za plastiki.

Charles aliwataka wanawake wengine kuiga mfano wa mke wake, aliyeanzia kazi ya kuokota makopo ya plastiki kwa kijihusisha na kazi halali bila kuona aibu, kufanya hivyo kutawafanya wawe na maendeleo kiuchumi.

"Vyuo vinazalisha wasomi wengi bila kujali kuwa kuna changamoto ya ajira, ni muda mwafaka kwa wasomi hao hasa watoto wa kike kutoona aibu kujiajiri wao wenyewe, kwani kuna kazi nyingi tu,siyo lazima kuokota makopo,mtu anaweza kuuza vitumbua,mkaa na akafanikiwa kimaisha,"alisema Charles.

Lucy Kipawa ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Oilcom, mbali na kumpongeza Mwanazaina, kuwa wakala wa makopo aliyeanzia kazi ya kuokota makopo ya plastiki, alisema kazi ya mama huyo imesaidia kutunza mazingira mtaani kwake.

Mwenyekiti huyo anasema Mtaa wa Oilcom ulliopo Nanenane Kata ya Tungi Manispaa ya Morogoro ni miongini mwa mitaa inayosifika kwa utunzaji wa mazingira na kwamba hiyo imesababishwa na kazi nzuri inayofanywa na Mwanasaina..

Fabian John mkazi wa Nanenane, aliwataka wanawake wengine kuingia mfano wa Mwanazaina, kufanya hivyo kutawakwamua kiuchumi, na kuondoka katika utegemezi na kutawafanya wamiliki mali zao wenyewe, ikiwemo ardhi maana watakuwa na uhakiki wa kipato.

